TAMKO KUHUSU KUKAMATWA NA KUENDELEA KUSHIKILIWA KWA MWANAHARAKATI NA METETEZI WA HAKI ZA BINADAMU, TITO MAGOTI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) pamoja na Mtandao wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu tunaendelea kuonesha masikitiko yetu kuhusiana na ukiukwaji wa haki za mtuhumiwa unaofanywa na Jeshi la Polisi dhidi ya mtetezi mwenzetu, Tito Magoti. Ni zaidi ya masaa 90 (siku nne) yamepita tangu ndugu Tito Magoti, Afisa Elimu kwa Umma wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kukamatwa na watu wasiojulikana. Tito alikamatwa mnamo Disemba 20, 2019 majira ya saa 4:30 maeneo ya Mwenge, jijini Dar es Salaam.

Baada ya wananchi kupaza sauti, Jeshi la Polisi kanda maalumu ya Dar es Salaam kupitia kwa kamanda Lazaro Mambosasa lilikiri kumshikilia Tito pamoja na watu wengine watatu kwa kile kilichodaiwa kuwa wanahojiwa na kuchunguzwa kwa makosa ya jinai ambayo hayakuwekwa wazi. Kauli ya kamanda Mambosasa imezua maswali kadhaa kwani haikuweka wazi kosa analoshutumiwa nalo wala kutaja kituo cha polisi anaposhikiliwa Tito. Baada ya taarifa ya kamanda Mambosasa wananchi, familia na wadau wa haki za binadamu walipata tumaini kwamba utakapofika muda wa kawaida wa kisheria wa masaa 24 baada ya mtuhumiwa kukamatwa, Tito na wenzake watafunguliwa jalada na kupata haki yao ya dhamana.

Hata hivyo, baada ya kupita kwa muda huo, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kwa kushirikiana na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu, familia na marafiki wa karibu wa Tito wamefika vituo mbalimbali vya polisi ikiwemo kituo kikuu cha polisi cha kati ambapo kote huko waliarifiwa kuwa Tito hayupo. Katika kuthibitisha hilo LHRC imewasiliana na uongozi wa juu wa jeshi la polisi akiwemo Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) ambaye pia ameonesha kutokuwa na taarifa sahihi juu ya alipo mpendwa wetu Tito Magoti.

Utaratibu uliotumika kumkamata Tito Magoti si utaratibu wa kawaida wa namna Jeshi la Polisi linavyotakiwa kufanya kazi. Namna ya ukamataji, mazingira aliyokamatwa na mwendelezo baada ya kukamatwa si hatua za kiweledi katika utendaji wa Jeshi la Polisi kuwashikilia watu bila taarifa na kutoa taarifa baada ya kelele za wananchi. Mazingira ya kukamatwa kwa Ndugu Tito yanaonekana yalikuwa ya kuviziwa, ya kutumia nguvu kupita kiasi, na bila kupewa haki za msingi ikiwemo kuwaarifu watu wake wa karibu kwamba anashikiliwa na Polisi.

Mambo haya yote yanazua maswali mengi na sintofahamu kwa wananchi na wadau wapenda haki hasa swala la Jeshi la Polisi kutokutaka kueleza umma na familia mahali alipo Tito Magoti hadi tunapoandika tamko hili siku ya nne. Imekuwa ni tabia inayozidi kukuwa nchini kwa kipindi kirefu sasa kwa vyombo vya usalama wa raia kukamata watuhumiwa kisirisiri kisha kubaki nao kwa muda mrefu bila ndugu wala jamaa kuwa na taarifa. Mifano ya karibuni ni pamoja na kukamatwa kwa Erick Kabendera (Mwanahabari), Maneno Mbunda (Wakili) na wengine.

Askari wanaodaiwa kumkamata Mtetezi Tito wanashutumiwa kwa kukiuka kanuni za ukakamataji wa watuhumiwa. Mfano hawakujitambulisha na walikuwa wamevaa kiraia na gari iliyotumika ilikuwa gari binafsi. Pia, nguvu iliyotumika wakati wa ukamataji ilikuwa ya ziada pasipokuwa na sababu za msingi tofouti na matakwa ya sharia.

Tamko la Jeshi la Polisi linalodai kuhusika na ukamatwaji wa Tito, linauthibitishia umma kwamba wanamshikilia Tito Magoti lakini leo siku ya nne sasa hawaruhusu wakili, ndugu wala mwajiri wake kumwona na kusimamia mahojiano yake kwa mujibu wa sheria.

Haki ya Dhamana

Ikumbukwe kwamba Jeshi la Polisi halina mamlaka ya kumshikilia mtuhumiwa kwa zaidi ya masaa 24 bila kumwachia kwa dhamana ya polisi au kumfikisha mahakamani. Haki ya dhamana ni haki ya Kikatiba ambayo raia yeyote anayo endapo kosa alilotenda linadhaminika kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi yetu. Lakini mpaka tunavyozungumza, Jeshi la Polisi limekaa na ndugu Tito kwa zaidi ya saa 24 na hajapewa dhamana na haijulikani yupo kituo gani cha polisi. Lengo kuu la uwepo wa Jeshi la Polisi ni kuhakikisha watuhumiwa

wanakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya maamuzi hasa Mahakama kwa kufuata taratibu za kisheria.

Haki ya kuhojiwa mbele ya mwanasheria na/au ndugu au jamaa wa karibu

Katika tamko la Jeshi la Polisi wamekiri kumshikilia Tito na watu wengine watatu kwa kile walichodai ni mahojiano na uchunguzi. Kwa hiyo Tito Magoti anahojiwa na Jeshi la polisi akiwa hana mwanasheria, ndugu wala mwajiri wake. Jambo hili linazua maswali mengi na kupelekea kuhoji nia ya la Jeshi la Polisi katika swala hili linaloleta taswira mbaya na kulipaka matope Jeshi letu. Madhara ya vyombo vya usalama kukiuka haki za raia ni makubwa kwani yanaleta chuki na huenda yakasababisha wananchi kutoshirikiana na vyombo hivyo kupelekea kuongezeka kwa matukio ya kujichukulia sheria mkononi na baadaye machafuko katika jamii.

Wito

i. Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya usalama vinawajibika kwa wananchi. Jeshi la Polisi litoe taarifa za alipo Tito Magoti ili aweze kupata haki zake kwa mujibu wa sheria au limwachilie kwa kuwa hadi sasa baada ya siku nne haijulikani anatuhumiwa kwa kosa gani.

ii. Jeshi la polisi ni chombo kilichowekwa kwa ajili ya ulinzi wa raia na mali zao, hivyo jeshi hilo halipaswi kutumika kuwakandamiza wananchi kwa namna yoyote ile.

iii. Asasi za Kiraia, watetezi wa haki za binadamu, waandishi, mahakama na wadau wote wapenda haki tunapaswa kusimama kwa pamoja kukemea matukio haya mabaya kwa Taifa haswa katika kipindi hiki ambacho ukiukwaji wa haki za binadamu umeshamiri.

iv. Wananchi tunapaswa kusimama na kuandamana dhidi ya ukiukwaji unaoendelea kufanywa na vyombo vya usalama dhidi ya watuhumiwa hapa nchini.

v. Kufuatia kukiri masuala kama haya, Tanzania tuhuishe mchakato wa Katiba ili kuweka chombo huru kitakachosimamia utendaji na uwajibikaji wa Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya usalama kwa lengo la kulinda Haki za Wananchi wakiwa mikononi mwa Polisi.

vi. Tunalitaka Jeshi la Polisi limwachilie au kumfikisha Tito na wenzake mahakamani leo tarehe 23/12/2019 kabla ya saa saba mchana, vinginevyo tutachukua hatua za kisheria za kimahakama kuwalazimisha kutii sheria zinazomlinda mtuhumiwa.

vii. Tunaendelea pia kusihi vyombo vingine vya utoaji haki hasa mahakama , kujitahidi sana kipindi hiki kujiweka huru zaidi, kufanya kazi kwa weledi, kulinda haki za wanyonge na kufanya kazi kwa misingi ya kikatiba, kisheria na haki za binadamu. Kimbilio pekee kwa mujibu wa Katiba pale haki zinapokiukwa ni Mahakama Kuu na Tume ya Haki za Binadamu, hivyo tunawasihi sana kutambua takwa hili la kikatiba na kulitenda kivitendo.

viii. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, nayo tunaikumbusha jukumu lake kikatiba la kulinda na kukemea ukiukwaji wa haki za raia. Kupitia Tamko hili tunaleta malalamiko rasmi kwenu kuhusu haki za watuhimiwa hapa nchini.

ix. Vyombo vya usalama viheshimu uhuru wa raia na watetezi wa haki za binadamu kutoa maoni yao juu ya mambo mbalimbali ya kitaifa na yenye maslahi kwa taifa.

Imetolewa na;

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)

na

Mtandao wa Wanawake Watetezi wa Haki za Binadamu (WHRDs)